KAULI YA MAELEZO YA CHANJO

# Chanjo ya Pneumococcal Conjugate: *Unayohitaji Kujua*

Many vaccine information statements are available in Swahili and other languages. See www.immunize.org/vis

Kauli nyingi za taarifa ya chanjo zinapatikana katika Kiswahili na lugha nyinginezo. Angalia www.immunize.org/vis

## 1. Je, kwa nini uchanjwe?

**Chanjo ya Pneumococcal conjugate** inaweza kuzuia **ugonjwa wa pneumococcal**.

**Ugonjwa wa pneumococcal** ni ugonjwa unaosababishwa na bakteria wa pneumococcal. Bakteria hawa wanaweza kusababisha aina nyingi za magonjwa, yakiwemo:

- Nimonia (maambukizi ya mapafu)
- Maambukizi ya sikio
- Maambukizi ya pua ya ndani
- Meningitis (maambukizi ya utandu unaofunika ubongo na uti wa mgongo)
- Bakteremia (maambukizi ya mkondo wa damu)

Mtu yeyote anaweza kupata ugonjwa wa pneumococcal, lakini watoto wadogo, watu wazima wazee, na watu walio na sababu fulani za hatari wako kwenye hatari kubwa zaidi.

Maambukizi mengi ya pneumococcal ni mepesi. Hata hivyo, zingine zinaweza kusababisha shida za muda mrefu, kama vile uharibifu wa ubongo au upotezaji wa kusikia. Meningitis, bakteremia, na nimonia inayosababishwa na ugonjwa wa pneumococcal inaweza kusababisha kifo.

## 2. Chanjo ya pneumococcal conjugate

Chanjo ya pneumococcal conjugate husaidia kulinda dhidi ya bakteria zinazosababisha ugonjwa wa pneumococcal. Kuna chanjo kadhaa za pneumococcal conjugate (PCVs). PCV mahususi na idadi ya dozi zinazopendekezwa zinategemea umri wa mtu, historia ya chanjo na hali ya matibabu. Mtoa huduma wako wa afya anaweza kukusaidia kuamua ni aina gani ya PCV, na dozi ngapi, zinapaswa kupokelewa.

- **Kwa kawaida watoto wachanga na watoto wadogo** wanahitaji dozi 4 za PCV. Dozi hizi zinapendekezwa kwa umri wa miezi 2, 4, 6 na 12-15.
- Baadhi ya **watoto wakubwa na vijana** ambao hawakupokea dozi zilizopendekezwa wakiwa watoto wachanga au watoto wadogo wanahitaji PCV. Hii inategemea umri na hali ya matibabu, au sababu zingine za hatari.
- **Watu wazima wenye umri wa miaka 19 hadi 49** ambao hawajapokea PCV na wana hali fulani za matibabu au sababu zingine za hatari wanapaswa kupokea PCV. Watu wazima wengine katika kundi hili ambao tayari wamepokea PCV wanaweza kupendekezwa wapokee dozi nyingine.
- **Watu wazima wenye umri wa miaka 50 au zaidi** ambao hawakupata PCV hapo awali wanapaswa kupokea chanjo ya PCV. Watu wazima wengine katika kundi hili ambao tayari wamepokea PCV wanaweza kupendekezwa wapokee dozi nyingine.

## 3. Zungumza na mtoa huduma wako wa afya

Mwambie mtoa huduma wako wa chanjo ikiwa mtu anayepokea chanjo:

- Amewahi kuwa na **athari ya mzio baada ya dozi ya awali ya aina yoyote ya PCV, au chanjo yoyote iliyo na diphtheria toxoid** (kwa mfano, DTaP), au ana **mzio wowote mkali, unaotishia maisha**

Kuna nyakati daktari wako anaweza kuamua kuchelewesha chanjo ya PCV hadi utakapokuja tena hospitalini siku nyingine.

Watu walio na magonjwa madogo, kama vile mafua, wanaweza kuchanjwa. Watu ambao ni wagonjwa kwa wastani au wagonjwa vibaya wanapaswa kwa kawaida kungojea hadi wapone.

Mtoa huduma wako wa afya anaweza kukupa habari zaidi.



U.S. CENTERS FOR DISEASE CONTROL AND PREVENTION

## 4. Hatari za mmenyuko unaotokana na chanjo

- Wekundu, uvimbe, maumivu, au wororo katika eneo lililodungwa; homa; kupoteza hamu ya kula; hasira (kukasirika); uchovu; maumivu ya kichwa; maumivu ya misuli; maumivu ya viungo; au baridi inaweza kutokea baada ya chanjo ya pneumococcal conjugate.

Watoto wadogo wanaweza kuwa katika hatari kubwa zaidi ya kupata degedege zinazosababishwa na homa baada ya PCV ikiwa inatolewa wakati mmoja na chanjo ya mafua isiyoamilishwa. Muulize mtoa huduma wako wa afya akupe maelezo zaidi.

Watu huzirai wakati mwingine baada ya taratibu za kimatibabu, ikiwemo kuchanjwa. Mwambie mtoa huduma wako ikiwa unahisi kizunguzungu au mabadiliko katika kuona kwako au kuhisi milio masikioni.

Kama ilivyo na dawa yoyote ile, kuna uwezekano mdogo sana kwa chanjo kusababisha mmenyuko mkali wa mzio, majeraha mengine mabaya, au kifo.

## 5. Je, itakuwaje ikiwa kuna tatizo baya sana?

Mmenyuko wa mzio unaweza kutokea baada ya mtu aliyechanjwa kuondoka kwenye kliniki. Ikiwa utaona dalili za mmenyuko mkali wa mzio (mabaka, kuvimba uso na koo, matatizo ya kupumua, moyo kupiga haraka, kizunguzungu, au udhaifu), piga simu **9-1-1** na umpeleke mtu huyo kwenye hospitali iliyo karibu.

Kwa dalili nyingine ambazo zinakupa wasiwasi, mpigie simu mtoa huduma wako wa afya.

Athari mbaya zinapasa kuripotiwa kwa Vaccine Adverse Event Reporting System [VAERS] (Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo). Mtoa huduma wako wa afya kwa kawaida ataandikisha ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe. Tembelea tovuti ya VAERS katika **www.vaers.hhs.gov** au piga simu **1-800-822-7967**. *VAERS ni ya kuripoti tu athari, na wafanyakazi wa VAERS hawatoi ushauri wa kimatabibu.*

## 6. National Vaccine Injury Compensation Program

National Vaccine Injury Compensation Program [VICP] (Mpango wa Kitaifa wa Ufidiaji wa Majeraha ya Chanjo) ni mpango wa serikali kuu ambao ulibuniwa ili kufidia watu ambao huenda walijeruhiwa na chanjo zingine. Madai kuhusiana na majeraha au vifo vinavyodaiwa kutokana na kuchanjwa yako na kikomo cha muda kwa kufaili, ambao unaweza kuwa mchache kama vile miaka miwili. Tembelea tovuti ya VICP katika **www.hrsa.gov/vaccinecompensation** au piga simu **1-800-338-2382** ili kujifunza kuhusu mpango huu na kufaili dai.

## 7. Je, ninawezaje kujifunza mengi zaidi?

- Muulize mtoa huduma wako wa afya.
- Pigia simu idara ya afya ya eneo lako au ya jimbo.
- Tembelea tovuti ya Food and Drug Administration [FDA] (Usimamizi wa Chakula na Dawa) ili upate machapisho ya vifurushi vya chanjo na taarifa ya ziada katika **www.fda.gov/vaccines-blood-biologics/vaccines**.
- Wasiliana na Centers for Disease Control and Prevention [CDC] (Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa):
  - Piga simu **1-800-232-4636** (**1-800-CDC-INFO**) au
  - Tembelea tovuti ya CDC katika **www.cdc.gov/vaccines**.

Swahili translation provided by Immunize.org